


# Jinsi Anansi Alipata Miguu Minane Myembamba


Brigid Simiyu
Wiehan de Jager

Kiswahili


African Storybook.org



Hapo zamani za kale, zamani sana, aliishi buibui mmoja aliyeitwa Anansi. Mke wa Anansi alikuwa mpishi mzuri. Anansi alipenda kuonja vyakula vilivyopikwa na wanawake wengine kijijini.



Siku moja, Anansi alipitia kwa Sungura, rafikiye mpendwa. Anansi aliona mboga chunguni. Alizipenda mboga hizo. Kwa msisimuko akasema, "Ninaona mboga chunguni." Sungura akamwambia, "Zitaiva hivi karibuni, subiri tule pamoja." Anansi alisema kwa haraka, "Samahani, ningependa sana kungoja, lakini nina haraka." Anansi alijua kwamba angekubali kusubiri, Sungura angempa kazi ya kufanya.



Anansi akamwabia Sungura, "Nitasokota utandu kisha nifunge ncha moja mguuni kwangu na nyingine chunguni. Mboga zitakapoiva, utauvuta utandu, nami nitakimbia nije." Sungura aliona hilo ni wazo zuri sana. Wakakubaliana kufanya hivyo.




Anansi alinukia chakula na kwa msisimko akasema, "Harufu tamu ya maharagwe yanayopikwa." Aliwaona Ngedere waliomwita, "Njoo tule maharagwe, bado kidogo tu yaive." Anansi akasema, "Ningependa sana tule pamoja, Baba Ngedere, lakini nina haraka." Kisha Anansi akasema atasokota utandu, afunge ncha moja mguuni mwake na ncha nyingine kwenye chungu cha maharagwe. Baba Ngedere na mtoto wake walikubali wazo hilo zuri.



Alipotoka kwa Ngedere, Anansi alinukia harufu ya chakula, akasema, "Nanusa harufu ya viazi vitamu na asali." Nguruwe akimwita, "Anansi, chungu changu kimejaa viazi vitamu na asali. Njoo tule." Anansi akajibu, "Ningependa lakini sina wakati." Kwa mara nyingine, Anansi akaamua asokote utandu, afunge ncha moja mguuni mwake na nyingine kwenye chungu cha viazi vitamu. Rafiki yake Nguruwe alikubali wakasokota utandu.



Anansi alipofika mtoni, miguu yake yote ilikuwa imefungwa kwa ncha za utandu. Anansi akawaza, "Hili lilikuwa ni wazo zuri sana. Ila najiuliza ni chungu kipi kitakachoiva kwanza?" Pale pale Anansi akasikia mguu mmoja umevutwa. Akasema, "Ah, hii ni ncha ya utandu uliofungwa kwenye chungu cha mboga."



Anansi aliendelea kusikia mvuto baada ya mwingine. Alivutwa pande tatu mara moja. "Ah! Jamani!" Anansi alisema alipovutwa kwa mara ya nne. Kabla hajapumua, akasikia ncha ya tano, ya sita, ya saba, na ya nane zikivutwa. Anansi alivutwa huku na kule. Kila mmoja alivuta ncha yake wakati ule ule. Miguu yake ilivutwa ikawa myembamba.



Anansi alijirusha mtoni kwa haraka. Tandu zote zilipochukuliwa na maji, alijivuta taratibu kwa maumivu hadi kando ya mto. Anansi aliugua kwa uchungu, "Ah! Ah!" Labda hili halikuwa wazo zuri kabisa." Siku ile hakupata chakula chochote. Tangu wakati huo, Anansi, Buibui, huwa na miguu minane myembamba."

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Jinsi Anansi Alipata Miguu Minane Myembamba

**Author** - Ghanaian folktale
**Translation** - Brigid Simiyu
**Illustration** - Wiehan de Jager
**Language** - Kiswahili
**Level** - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
**Source** www.africanstorybook.org